

Sababu Zinazoukilia Matumizi ya Tungo za Utendeka na Utendwa katika Lugha ya Kiswahili

**Fredrick Emanuel Kuyenga
Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

fredrickkuyenga@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza tungo za utendeka na utendwa katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, yapo madai miongoni mwa wanaisimu mbalimbali kwamba, tungo hizo zinafanya kazi inayofanana katika lugha kisarufi; yaani kupunguza kishiriki kimoja cha kitenzi katika muundo wa vishiriki vya kitenzi (Khamisi, 1972; Rugemalira, 1993; na Mkude, 2005). Data za utafiti huu zilipatikana kwa njia ya usomaji wa nyaraka pamoja na usaili. Uchanganuzi wa data umetumia misingi ya mkabala wa Sarufi Leksia Amilifu ulioasisiwa na na Bresnan na Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba utendeka na utendwa ni tungo mbili tofauti kimuundo na kiuamilifu katika lugha ya Kiswahili. Aidha, imebainika kwamba ziko sababu kadhaa zinazoukilia utokeaji wa tungo hizo: muundo wa vishiriki vya kitenzi, upatanisho wa kisarufi, kuondoa mtenda katika tungo, umadaishaji wa kiathirika, ufokalishaji wa mtenda, ukwezaji wa mmiliki na kuondoa utata katika lugha. Kutokana na matokeo haya, inapendekezwa kwamba, utafiti zaidi kama huu ufanyike katika lugha nyingine za Kibantu ambazo hazijafanyiwa utafiti ili kulinganisha na kutofautisha sababu za utumikaji wake katika lugha ya Kiswahili na lugha lugha zingine za Kibantu.

Dhana za Msingi: Tungo, utendeka, utendwa, vishiriki vya kitenzi

Utangulizi

Makala hii inabainisha na kufafanua sababu zinazoukilia matumizi ya tungo za utendeka na utendwa katika lugha ya Kiswahili. Tungo za utendeka ni tungo zinzoashiria kuhusu mambo kadhaa; kwanza, ufanyikaji wa tendo bila kuwapo mtendaji wa tendo. Pili, uwezekano wa tendo kufanyika. Tatu,

zinaelezea kuhusu matokeo ya tendo husika. Tungo hizo zinaashiriwa na mofu *-ik-* kama katika *lim-ik-a*, *-ek-* katika *chez-ek-a*, na *-k-* katika *chomo-k-a* katika kitenzi kiundacho tungo. Kwa upande mwingine, tungo za utendwa ni tungo zinazoelezea kuwa kiima kina uamilifu wa kutendwa; yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani na kinaathiriwa moja kwa moja na tendo linalofanywa na kiima cha tungo tenda (Mkude, 2005). Katika lugha ya Kiswahili tungo hizi zinaashiriwa na mofu *-w-* kama katika *lim-w-a* katika kitenzi ndani ya tungo hizo.

Vilevile, tungo za utendeka na utendwa zinaondoa kishiriki kimoja katika muundo wa vishiriki vya kitenzi katika tungo. Yaani, tungo zote mbili, zinafanya kazi ya kupunguza kishiriki kimoja cha kitenzi katika muundo wa vishiriki vya kitenzi, katika utendwa kinaweza kurejeshwa kama oblikyu (Rugemalira, 1993; Mchombo, 1995; Mkude, 2005; Khamisi, 2008; Kaoneka, 2009; Simango, 2009; na Lusekelo, 2012). Kishiriki kinachoondolewa ni kile ambacho kinarejelea mtenda katika tungo. Kishiriki hicho, chenye dhima tenda katika tungo za utendeka, kinaondolewa kabisa katika muundo wa vishiriki vya kitenzi. Lakini, katika tungo za utendwa, kinaweza kurejeshwa na kuwa chagizo au oblikyu. Kwa muktadha huo, kama tungo hizi zote zinafanya kazi inayofanana ya kupunguza kishiriki kimoja katika lugha, kwa nini tungo zote mbili zinahitajika katika muundo wa lugha kimawasiliano? Swali hili linaibua changamoto kitaaluma kuhusu uamilifu wa kila mojawapo ya tungo hizo katika lugha. Kwa sababu hiyo, uchunguzi huu unabainisha sababu zinazokilia matumizi ya tungo hizo katika lugha ya Kiswahili ili kujua kwa nini tungo zote mbili zinahitajika katika muundo wa lugha kimawasiliano.

Kiunzi cha Nadharia

Uchunguzi na ufafanuzi katika makala hii umeongozwa na Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (SLA). Nadharia hii iliasisiwa na Joan Bresnan pamoja na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii inazingatia ufafanuzi wa vipengele vya lugha kwa kutumia taarifa za kileksika na uamilifu wa viambajengo vya sentensi. Vilevile, inahusisha miundo mbalimbali ya sentensi kwa kutumia kanuni. Miundo hiyo ni muundo amilifu (MAM) ambao unaonesha dhima za kisarufi (DhK) za viambajengo vya sentensi pamoja na sifa za kimofosintaksia za viambajengo hivyo. Dhima hizo za kisarufi ni kiima, yambwa, yambiwa, oblikyu, kijalizo, na chagizo. Dhima hizi zinaashiriwa na sifa za kimofolojia, kisintaksia, na kisemantiki katika lugha za Kibantu. Mathalani, kiima kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kipatanishi cha kiima. Yambwa ina sifa ya kuwekewa kiambishi yambwa katika kitenzi au kuwa kiima cha sentensi tendwa. Pia, kuna muundo wa vishiriki vya kitenzi (MVSH) ambao unaonesha idadi na dhima za kisemantiki (DhKI) za vishiriki vya kitenzi Muundo huu unaonesha idadi ya vishiriki katika kitenzi na dhima zake kisemantiki. Dhima za kisemantiki ni kama vile mtenda, kithimu na kimahali. Mathalani, kitenzi *tia* kinahitaji vishiriki vitatu ambavyo ni mtiaji (mtenda), kinachotiwa (kithimu), na mahali (kimahali). Kwa hiyo, MVSH wa kitenzi *tia* ni <mtenda, kithimu, kimahali>. Dhima za kisemantiki zinahusishwa na dhima za kisarufi kwa kuzingatia masuala matano.

Kwanza, ***udarajia wa dhima za kisemantiki***, yaani mpangilio wa dhima za kisemantiki kulingana na uwezo wa dhima husika kuwa kiima kuliko dhima nyingine katika udarajia. Mathalani, Mkude (2005) anapendekeza udarajia wa dhima za kisemantiki katika Kiswahili kuwa ni:

Mtenda=>Eksiperiensa=>Mpokeaji=>Mnufaika=>Kithimu=>Kiathirika=>Kimahali=>Kifaa. Kwa kuzingatia udarajia huu, dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya juu ndiyo inayoweza kuwa kiima kuliko ile iliyopo katika nafasi ya chini. Mathalani, kithimu kinapaswa kuwa kiima na siyo kimahali. Hata hivyo, kuna wakati kimahali ambacho kipo katika nafasi ya chini kinapandishwa hadhi na kuwa kiima licha ya kuwapo kwa kithimu. Upandishwaji wa hadhi ya kimahali hutokea iwapo kimahali ni mada katika sentensi.

Pili, ni *ufafanuzi wa dhima za kisarufi* kwa kutumia sifa bainifu. Hivyo, kwa mujibu wa SLA, kiima ni dhima inayofanywa na neno au kirai kisichohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki.

Tatu, ni *kanuni ya uhusishaji kimajumui* ambapo mtenda anahusishwa na sifa ya kuwa kiima au oblikyu, kithimu kinahusishwa na sifa ya kuwa kiima au yambwa, na kimahali kinahusishwa na sifa ya kuwa kiima au oblikyu.

Nne, ni *michakato ya kimofolojia* ambayo inaongeza au kupunguza idadi ya vishiriki vya kitenzi. Michakato hiyo ni kama vile uambikaji wa kiambishi cha utendeka au utendwa. Michakato hii inasababisha kufanyika kwa miundo ya vitenzi inayokubali na ile isiyokubali utokeaji wa tungo za utendeka na zile za utendwa.

Tano, ni *sharti la ukubalifu* ambalo lina kanuni ndogo mbili. Kanuni ya *kiima* inayohitaji kwamba kila tungo lazima iwe na kiima na kanuni ya *uwiano-dhima* inayohitaji kwamba kila dhima moja ya kisemantiki ihusishwe na dhima moja ya kisarufi. Nadharia hii pia inahusisha muundo wa taarifa (MT). Kila tungo ina muundo wake wa taarifa kimawasiliano.

Taarifa kuu zinazowasilishwa katika tungo ni ‘mada’ na ‘fokasi’. Mada ni taarifa inayojulikana kwa mtoaji na mpokeaji wa taarifa kutokana na muktadha wa mawasiliano. Taarifa ya aina hii hupewa kipaumbele katika tungo, ambayo mara nyingi huwa ni kiima cha tungo. Fokasi ni sehemu ya tungo inayotoa taarifa mpya katika tungo. Hali hii imedhihirika wazi kutokana na data zilizokusanywa kutoka katika usomaji wa nyaraka na usaili.

Kwa ujumla misingi ya nadharia ya SLA imesadia katika ufafanuzi wa data za utendeka na utendwa kwa kutumia ujuzi binafsi pamoja na kiunzi cha nadharia kwa kuzingatia sifa za MVSH, Dhima za kisarufi, dhima za kisemantiki na Muundo wa Taarifa wa tungo hizo.

Methofolojia ya Utafiti

Hoja na data za zilizowasilishwa katika makala hii zilipatikana kutoka maktabani na uwandani. Data za maktabani zilikusanywa katika magazeti ya Mwananchi na Nipashe ya kati ya mwezi Machi - Oktoba 2020. Data hizo zilipatikana kwa njia ya usomaji wa nyaraka (magazeti tajwa) ambapo mtafiti alikusanya tungo za utendeka na utendwa kwa kuzingatia muktadha zilimojitokeza pamoja na sifa zake kwa lengo la kupata tungo hizo pamoja na sababu za utumikaji wake. Kwa kila gazeti tajwa alichukua nakala 30 ambazo zilikuwa zimetumia kwa wingi tungo za utendeka na utendwa ikilinganishwa na tungo za aina zingine. Aidha, data za uwandani zilipatikana kwa njia ya usaili. Data hizo zilikusanywa kutoka kwa wahariri wawili wa magazeti tajwa. Lengo ni kujua sababu zilizowasukuma wahariri hao kutumia tungo za utendeka na utendwa kwa wingi katika mijadala na taarifa mbalimbali zinazoibuliwa katika magazeti husika ikilinganishwa na tungo nyinginezo.

Matokeo ya Utafiti

Ubainishaji wa sababu zinazoukilia matumizi ya tungo za utendeka na utendwa katika makala hii umefanyika kwa kuzingatia MVSH vya kitenzi, dhima za kisarufi, dhima za kisemantiki, sifa za kimofosintaksia za viambajengo na muundo wa taarifa. Sababu kadhaa zimebainishwa: Kwanza, ni MVSH vya kitenzi. Pili, kuondoa mtenda katika tungo. Tatu, kuleta upatanisho wa kisarufi. Nne, ukwezaji wa mmiliki. Tano, kuondoa utata. Sita, ufokalishaji wa mtenda na saba ni umadaishaji wa kiathirika/kithimu. Sehemu inayofuata imejadili na kufafanua sababu zinazoukilia matumizi ya tungo hizo katika lugha ya Kiswahili.

Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi Husika (MVSH)

Kwa mujibu wa SLA, matumizi ya tungo za utendeka na zile za utendwa yanaukiliwa na MVSH vya kitenzi kinachohusika katika tungo kimawasiliano. Katika lugha, vitenzi vina miundo mbalimbali ya vishiriki. Ipo miundo inayoruhusu na ile isiyoruhusu utokeaji wa tungo husika katika lugha kimawasiliano. Kwa mfano, kitenzi ambacho muundo wake unahusisha mtenda hakikubali kuambatana na dhima hiyo kama chagizo katika tungo za utendeka kama inavyoonekana katika Mfano Na. (1).

- (1) (a) *Mw-alimu* [a-me-fukuz-w-a (na **waziri**)
kng1-alimu kk1-tmlf-fukuz-ktndw-kt (na kng1.waziri)
'Mwalimu amefukuzwa (na waziri).'
(b) *Mw-alimu* a-me-fukuz-ik-a (na **waziri**)*
kng1-alimu kk1-tmlf-fukuz-ktndk-kt (na kng1.waziri)
'Mwalimu amefukuzika.'


Mfano Na. (1a) unaonesha tungo ya utendwa ambayo ina kiathirika *mwalimu* na mtenda *waziri*. Mfano Na. (1b) unaonesha tungo ya utendeka.

Tungo hiyo haikubali kutokea pamoja na mtenda *waziri* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. (1).

Kielelezo Na. 1: Dhima za Kisarufi na za Kisemantiki katika Tungo za Utendeka na Utendwa

*Mwalimu amefukuzika (na waziri)**

Mwalimu amefukuzwa (na waziri)



Kielelezo Na. (1) kinaonesha kuwa kitenzi cha utendeka **fukuzika* kina kiathirika *mwalimu* bila mtenda *waziri*. Aidha, kikiambatana na mtenda tungo zalishwa haikubaliki kisarufi. Kitenzi cha utendwa *fukuzwa* kina kiathirika *mwalimu* na mtenda *waziri*. Kwa mujibu wa DhK na DhKI, kiathirika *mwalimu* ni kiima, mtenda *waziri* ni chagizo. Hivyo, mtumiaji wa lugha husika itamlazimu kutumia muundo wa tungo ya utendwa ili kuwasilisha taarifa ambayo inahusisha mtenda kama chagizo. Ikumbukwe kwamba, ili tungo ya utendeka itokee na kukubalika kisarufi muundo wake wa vishiriki, haupaswi kuwa na dhima ya mtenda ikilinganishwa na ile ya

utendwa ambayo inakubali kuambatana na dhima hiyo katika muundo wake wa vishiriki.

Kuondosha Mtenda katika Muundo wa Tungo

Kwa kutumia dhana ya muundo wa vishiriki vya kitenzi (MVSH), lengo mojawapo la kutumia tungo za utendeka katika tungo kimawasilino ni kumwondoa mtenda wa tendo katika muundo wa kitenzi cha tungo (Khamisi, 1972; Rugemalira, 1993; na Mkude, 2005). Hivyo, muundo wa kitenzi unabakia na kishiriki kimoja ambacho ni kiathirika au kiambajengo chochote kinachorejelea dhima nyingine yoyote yenye uamilifu sawa na ule wa kiathirika katika tungo. Hii ni kwa sababu, mtumiaji wa lugha anachagua kutumia tungo za utendeka endapo hataki kujiingiza kwenye changamoto ya kumtaja mtendaji wa tendo katika tungo. Zipo sababu kadhaa zinazomsukuma mtumiaji wa lugha kutomtaja mtenda huyo katika tungo: sababu ya kwanza, ni kama mtendaji wa tendo hajulikani katika muktadha wa mawasiliano. Katika maisha ya kila siku, kuna matukio ambayo mtendaji wake hajulikani hasa katika makosa ya jinai. Hivyo utendeka au utendwa usiohusisha mtendaji wa tendo unakuwa ndiyo njia nzuri ya kueleza matukio kama hayo katika lugha kama inavyoonekana katika Mfano Na. (2).

- (2) (a) *We-zi wa-me-harib-u bomba la mafuta*
Kng2-zi kk2-tmlf-harib-kt kng5.bomba la kng6.mafuta
'Wezi wameharibu bomba la mafuta.'
- (b) *Bomba la mafuta li-me-harib-ik-a (na we-zi)**
kng5.bomba la mafuta kk5-tmlf-harib-ktndk-kt na
kng2-zi
'Bomba la mafuta limeharibika.'

Sababu Zinazoukilia Matumizi ya Tungo za Utendeka na Utendwa

- (c) *Bomba la mafuta* *li-me-harib-i-w-a (na we-zi).*
kng5.bomba la mafuta kk5-tmlf-harib-ktndea-ktndw-kt
(na kng2-zi)
'Bomba la mafuta limeharibiwa'


Mfano Na. (2a) unaonesha tungo ya utenda yenye mtenda *wezi* na kiathirika *bomba la mafuta*. Mfano Na. (2b) unaonesha tungo ya utendeka yenye kiathirika *bomba la mfuta* bila mtenda. Tungo hiyo ikiambatana na mtenda *wezi* haikubaliki kisarufi. Mfano Na. (2c) unaonesha tungo ya utendwa ambayo ina kiathirika *bomba la mfuta* na mtenda *wezi* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. (2).

Kielelezo Na. 2: Dhima za Kisarufi na za Kisemantiki katika Tungo za Utendeka na Utendwa

Wezi wameharibu bomba la mafuta

*Bomba la mafuta limeharibika (na wezi)**

Bomba la mafuta limeharibiwa (na wezi)



Kielelezo Na. (2) kinaonesha kuwa kitenzi cha utenda *haribu* kina mtenda *wezi* na kiathirika *bomba la mafuta*. Mtenda ni *kiima* na kiathirika ni *yambwa*. Halikadhalika, kitenzi cha utendeka **haribika* kina kiathirika *bomba la mafuta* bila mtenda *wezi*. Aidha, kikiambatana na mtenda tungo zalishwa haikubaliki kisarufi. Kitenzi cha utendwa *haribiwa* kina kiathirika *bomba la mafuta* na mtenda *wezi* ameondolewa katika muundo wa vishiriki.

Kitenzi hicho kinaweza kuondolewa dhima ya mtenda na kubakia na muundo sawa na ule wa utendeka. Hii ni kwa sababu kiambajengo kinachorejelea mtenda ni cha hiari katika tungo hizo. Kwa mujibu wa DhK, kiathirika *bomba la mafuta* ni kiima na mtenda *wezi* ni chagizo.

Pili, kama mtendaji wa tendo anafahamika kulingana na anaphora na katafora. Kuna baadhi ya mikitadha tungo zimeunganishwa kwa namna ambayo inawezekana kubashiri mtendaji wa tendo kutokana na muktadha. Kwa hiyo, hakuna haja ya mtumiaji wa lugha kumtaja mtendaji wa tendo katika tungo ya utendeka au ile ya utendwa kama mtendaji huyo anaweza kufahamika kwa urahisi kutokana na muktadha wa mawasiliano katika matini husika kama inavyoonekana katika Mfano Na. (3).

- (3) (a) ***Mvua kubwa i-li-ny-esh-a usiku kucha. Nyumba zote za udongo zi-me-bomol-ek-a*/zi-me-bomol-e-w-a***

‘Mvua kubwa ilinyesha usiku kucha. Nyumba zote za udongo zilibomoka/zilibomolewa.’

- (b) ***M-toto m-moja a-li-kuwa a-na-chez-e-a vy-ombo kabati-ni. Kando y-ake, ku-li-kuwa na sahani i-me-vunj-ik-a/i-me-vunj-w-a***

‘Mtoto mmoja alikuwa anachezea vyombo kabatini. Kando yake, kulikuwa na sahani imevunjika/imevunjwa.’

Katika Data Na. (3a), kirai kitenzi cha tungo ya utendeka na utendwa ‘*zilibomoka/zilibomolewa*’ hakina mtenda aliyetajwa katika kishazi hicho. Kwa kuwa kishazi hicho kimetanguliwa na kishazi kingine ambacho kisemantiki kina uhusiano nacho inaweza kufahamika kwa urahisi kwamba

mojawapo ya kirai nomino kilichopo kwenye kishazi cha mwanzo ndicho kirai nomino kinachorejelea mtendaji wa tendo katika kishazi kinachofuata cha tungo ya utendeka na ile ya utendwa. Kwa muktadha huo ni *mvua*. Ndivyo ilivyo katika tungo Na. (3b) ambapo kirai nomino kinachorejelea mtendaji wa tendo ni '*mtoto mmoja*' ndivyo ilivyo kwa tungo zote mbili. Hapa tungo za utendwa zinaonekana kukubalika zaidi kisarufi kuliko zile za utendeka ambazo zinanekana kuzua utata wa kisemantiki kwa kiwango fulani.

Tatu, kama mtendaji wa tendo kwa asili anatabirika hakuna haja ya kumtaja katika tungo. Kuna vitu vya asili au vya kisheria ambavyo kazi zake zinajulikana. Kwa hiyo hakuna haja ya kuvitaja katika muundo wa tungo labda kuwe na sababu ya msingi ya kufanya hivyo, kama vile ufokalishaji kama inavyoonekana katika Mfano Na. (4).

- (4) (a) *Wa-toto wa-nyony-esh-ek-a*/ wa-nyony-esh-w-e* kwa *mi-aka mi-wili*.

'Watoto wanyonyesheka/ wanyonyeshwe kwa miaka miwili.'

- (b) *A-me-tup-ik-a*/ a-me-tup-w-a* jela *mi-aka mi-tatu* kwa *w-izi*.

'Ametupika/ametupwa jela miaka mitatu kwa wizi.'

Data Na. (4a) inadhihirisha kuwa kazi ya unyonyeshaji inaweza tu kufanywa na aina moja ya kundi la watu ambao wanajulikana vizuri *wazazi wa kike*. Kuwataja ni kuongeza uradidi katika tungo kama ilivyo katika Data Na. (4b) inavyoonesha kazi ya kuhukumu watu ni *mahakimu* tu na *majaji* ndiyo wanafanya hivyo. Umma unalijua hili. Hakuna umuhimu wa

mtumiaji wa lugha kuwataja watendaji hao isipokuwa tu kama kuna muktadha unaohitajia kufanya hivyo. Njia nzuri hapa inayofaa kutumika ni kutumia tungo za utendwa ambazo hazina utata wa kisemantiki ikilinganishwa na zile za utendeka.

Nne, kama kumtaja mtendaji wa tendo kutaleta mgogoro au kutaathiri uelewa wa jambo husika basi mtenda huyo anaondolewa katika tungo. Hii inahusika sana katika mikitadha ya kisayansi na kitaaluma ambapo weledi unasisitizwa bila kujali cheo au sifa ya wahusika wa tukio ili kutunza siri au kulinda imani ya watu katika taaluma husika. Hapa mchakato ndiyo unatakiwa kutawala au kuzungumza na siyo mtendaji kama inavyoonekana katika Mfano Na. (5).

- (5) (a) *Vi-pimo vi-wili vya dawa **vi-li-changany-ik-a***/ **vi-li-changany-w-a** na vi-pimo vi-tatu vya maji.*

‘Vipimo viwili vya dawa vilichanganyika/vilichanganywa na vipimo vitatu vya maji.’

- (b) *Vi-pimo vi-wili vya malaria **vi-li-fany-ik-a***/**vi-li-fany-w-a** na vi-pimo vi-tatu vy-a UKIMWI.*

‘Vipimo viwili vya malaria vilifanyika/ vilifanywa na vipimo vitatu vya UKIMWI.’

Data Na. (5) zinaonesha kuwa mchakato ndiyo unatakiwa kutawala na siyo mtendaji wa tendo. Mchakato huo unatoa kipaumbele kwa tungo za utendwa kutumika zaidi kuliko zile za utendeka ambazo zina utata wa kisemantiki.

Tano, mtenda huondolewa katika tungo kwa lengo la kuokoa muda na nafasi. Taarifa inayoweza kuwasilishwa kwa maneno mawili haihitaji kuwasilishwa kwa maneno mengi hasa katika ulimwengu huu wa kidijitali kama tungo inajitosheleza. Kumuondoa mtenda kunaokoa nafasi na muda katika mawasiliano. Katika dunia ya sasa inasisitizwa kueleza wazo kwa ufupi kwa kadri iwezekanavyo. Kwa hiyo njia yoyote iwe ya kiisimu au nyinginezo zinazoweza kusaidia ili kueleza kwa ufupi hasa katika vyombo vya habari inapaswa kutumiwa kama inavyoonekana katika Mfano Na. (6).

- (6) (a) *Wa-tu 16 wa-me-bak-w-a*
kn2-tu 16 kk2-tmlf-bak-ktndw-kt
'Watu 16 wamebakwa.'
- (b) *Wa-tu 16 wa-me-bak-ik-a**
kng2-tu 16 kk2-tmlf-bak-ktndk-kt
'Watu 16 wamebakika.'
- (c) *Wa-nawake 15 wa-me-kut-w-a (na dawa za kule-vy-a)*
kng2-nawake 15 kk2-tmlf-kut-ktndw-kt (na kng9.dawa za suk-le-ktndsh-kt)
'Wanawake 15 wamekutwa (na dawa za kulevya).'
- (d) *Wa-nawake 15 wa-me-kut-ik-a (na dawa za kulevya)**
kng2-nawake 15 kk2-tmlf-kut-ktndk-kt (na kng9.dawa za suk-le-ktndsh-kt)
'Wanawake 15 wamekutika (na dawa za kulevya).'

Data Na. (6) inaonesha kuwa mhariri ametumia mbinu ya namba na kumuondoa mtendaji wa tendo ili kuokoa muda na nafasi katika gazeti.

Vilvile, hutumika kwa lengo la kushawishi kibiashara. Kwa mfano, katika magazeti tajwa tungo hizo zimetumika ili kumvutia msomaji anunue gazeti na kufuatilia habari husika kwa kuficha mtendaji wa tendo katika vichwa vya magazeti. Hivyo, mtumiaji wa lugha hapa atachagua kutumia muundo wa tungo ya utendwa zaidi kuliko ile ya utendeka ambayo inaonekana kuwa na changamoto ya kisemantiki kwa lengo la kutomtaja mtendaji wa tendo katika tungo ili kufikisha taarifa anayoiwasilisha kwa mpokeaji bila changamoto yoyote ya kimawasiliano. Hapa tungo za utendwa zinakuwa ni mwafaka zaidi kutumika ikilinganishwa na zile za utendeka. Utendeka unatumika tu katika mazingira ambayo hakuna changamoto za kimawasiliano kama ilivyo katika Mfano Na. (6) hapo juu.

Kuleta Upatanisho wa Kisarufi katika Matini (Ushikamani)

Matumizi ya tungo za utendeka na utendwa yameegemea zaidi katika muktadha wa kimawasiliano. Yanahusiana na mbinu ya uundaji wa taarifa na mpangilio wake katika matini. Mara nyingi inahusisha kuondoa baadhi ya taarifa ambazo zinafanana na ambazo zinaweza kuelezwa kwa kutumia taarifa zingine na kutoa fasiri nzuri. Hii inatokea mara nyingi katika michakato ya kisintaksia ambayo inajumuisha urejeleaji katika uunganishaji na urejeshaji. Taarifa ambayo inahusiana na ya awali mara nyingi hurejeshwa au kuunganishwa au kufokalishwa, wakati taarifa mpya inaelezwa wazi au inapewa kipaumbele. Kinafasi, taarifa ya ufokalishaji inakuwa mwishoni mwa tungo wakati inayojulikana inaanza mwanzoni mwa tungo. Uundaji huu wa tungo ni wa muhimu katika kuleta masikizi mazuri ya mtiririko wa maneno katika tungo. Utendwa una sifa ya ufokalishaji wa kiima cha tungo tenda kuwa chagizo cha tungo ya utendwa. Hivyo, kutumia utendwa inaweza kuwa njia nzuri ya kuleta ushikamani

katika matini kuliko kutumia utendeka kama inavyoonekana katika Mfano Na. (7a).

(7) (a) ***Mw-alimu a-li-ugu-a ghafla, i-ka-bidi a-kimbi-z-w-e hospitali-ni***

kng1-alimu kk1-knj-ugu-kt ghafla, kk9-knj-bidi kk1-kimbi-ktndsh-ktndw-kt kng9.hospitali-ktm

‘Mwalimu aliugua ghafla, ikabidi akimbizwe hospitalini.’

(b) ***Mw-alimu a-li-ugu-a ghafla, i-ka-bidi a-ki-mbi-z-ik-e hospitalini****

kng1-alimu kk1-knj-ugu-kt ghafla, kk9-knj-bidi kk1-kimbi-ktndsh-ktndk-kt kng9.hospitali-ktm

‘Mwalimu aliugua ghafla, ikabidi akimbizike hospitalini.’

Data Na. (7a) inadhihirisha kuwa matumizi ya kauli ya utendwa katika kishazi cha pili *akimbizwe* katika tungo hiyo yanaruhusu uhamishaji wa kishiriki ambacho ni yambwa (mwalimu) katika nafasi ya kiima ili kuwezesha udondoshaji wa kirai hicho katika kirai cha pili kwa sababu kinafanana na kishiriki kilichopo katika kirai cha kwanza katika tungo. Tungo hiyo isingesikika vizuri, kama ingebadilishwa na kuwa katika utendeka au utenda kama inavyoonekana katika Mifano Na. (8b) & (8c) mtawalia.

(8) (c) ***Mw-alimu a-li-ugu-a ghafla, i-ka-bidi wa-tu wa-m-kimbi-z-e mw-alimu hospitali-ni***

kng1-alimu kk1-knj-ugu-kt ghafla, kng9-knj-bidi kng2-

tu kk2-ky-kimbi-ktndsh-kt kng1-alimu kng9.hospitali-
ktm

‘Mwalimu aliugua ghafla, ikabidi watu wamkimbize
mwalimu hospitali.’

Katika muktadha wa Mfano Na. (8c), ili kuhakikisha kwamba kuna urari mzuri wa taarifa, ni lazima, wakati wote, kuhakikisha kwamba virai vinavyofanya kazi inayofanana katika tungo vinaunganishwa. Hii inahusisha kuvigeuza virai vilivyounganishwa katika utendwa na siyo katika utendeka ambapo tungo zalishwa inakuwa haikubaliki kama ilivyo katika Mfano Na. (9).

- (9) (a) **Jeni a-li-mu-omb-a baba y-ake kng10.shilingi mia a-
ka-p-e-w-a** mia mbili

kng1.Jeni kk1-knj-ky1-omb-kt kng1.baba kv1-ake
kng9.shilingi kv10.mia kk1-knj-p-kntdea-ktndw-kt
kngkv10.mia kv10.mbili

‘Jeni alimwomba baba yake shilingi mia akapewa mia
mbili.’

- (b) **Musa a-li-ib-a kuku, a-ka-fung-w-a mi-ezi mi-wili na
ku-chap-w-a** vi-boko 5.

kng1.Musa kk1-knj-ib-kt kng1.kuku, kk1-knj-fung-
ktndw-kt kng9-ezi kv9-wili na suk-chap-ktndw-kt
kng8-boko kv8-boko kv-5

‘Musa aliiba kuku, akafungwa miezi miwili na
kuchapwa viboko 5.’

- (c) **Jeni a-li-mu-omb-a baba y-ake shilingi mia a-ka-p-ek-**

*a mia mbili**

kng1.Jeni kk1-knj-ky1-omb-kt kng1.baba kv1-ake
kng9.shilingi kv9.mia kk1-knj-mz-ktndk-kt kng9.mia
kv9-mbili

‘Jeni alimuomba baba yake shilingi mia akapeka mia
mbili.’

(d) *Musa a-li-ib-a kuku, a-ka-fung-ik-a mi-ezi mi-wili na
ku-chap-ik-a vi-boko 5**

kng1.Musa kk1-knj-ib-kt kng1.kuku, kk1-knj-fung-
ktndk-kt kng9-ezi kv9-wili na suk-chap-ktndk-kt kng8-
boko kv8-boko kv-5

‘Musa aliiba kuku, akafungwa mezi miwili na
kuchapika viboko 5.’

Data Na. (9a) & (9b) zinaonesha kuwa kama mtumiaji wa lugha atahitaji kuwasilisha taarifa ambayo iko katika mfumo wa aina hiyo ya matini, itamlazimu kutumia tungo za utendwa kuunganisha tungo zenye virai vinavyofanana kiuamilifu ili kuleta upatanisho mzuri wa kisarufi (ushikamani) kuliko kutumia utendeka kama ilivyo katika Data Na. (9c) & (9d). Hii itasaidia kuzalisha tungo zinazokubalika kimuundo na kiuamilifu katika sarufi ya lugha ya Kiswahili.

Uakisiwaji wa Mfumo Msonge wa Nomino Kisarufi (Ukwezaji wa Mmiliki)

Umsonge wa nomino unaonekana kuwa jambo la kawaida katika lugha ya binadamu (Bentley, 1994: 129 na Keenan, 1985). Aidha, hauishii tu katika tofauti za matabaka ya watu kijamii, bali unaendelea hadi katika udarajia wa vitu wanavyojishughulisha navyo, ikijumuisha maneno wanayoyaunda

kama vile nomino. Kuna baadhi ya lugha ambazo zina mipaka kuhusiana na kirai nomino kipi kiwe katika nafasi ya kiima katika MVSH vya kitenzi katika muktadha mahususi. Katika Kiswahili, kwa mfano, siyo jambo la kushangaza kuwa na vishiriki vilivyoko chini katika msonge wa nomino kuchukua nafasi ya juu katika tungo kuliko vile vilivyopo juu katika msonge huo (Mkude, 2005). Hata hivyo, hili ni kweli tu katika vishiriki vinavyohusu binadamu ambaye anafaidi upendeleo wa aina fulani kisintaksia, kama vile ukwezaji wa mmiliki. Kwa hiyo, kama mtumiaji wa lugha anataka kuzingatia sarufi ya lugha husika, atatumia tungo za utendwa ili kuakisi kanuni hii ya kisarufi katika lugha. Kwa mfano, kama kiima cha tungo ya utenda ni kitu kinachomilikiwa, mmiliki kisarufi ndiye anakuwa yambwa. Njia inayokubalika ni kubadili muundo wa uwasilishaji na kukifanya kimiliki kuwa kiima katika tungo za utendwa. Kwa muktadha huo, utendwa ndiyo inakuwa njia nzuri ya kuaksi ukwezaji wa mmiliki kuliko utendeka kama inavyoonekana katika Mfano Na. (10).

(10) (a) *A-na-sumbul-i-w-a* (*na ma-cho*)

kk1-knj-sumbul-ktndea-ktndw-kt na kng6-cho

‘Anasumbuliwa na macho.’

(b) *A-na-sumbul-ik-a* (*na ma-cho*)*

kk1-knj-sumbul-ktndk-kt (na kng6-cho)

‘Anasumbulika (na macho).’

Ma-cho ya-na-m-sumbu-a

kng6-acho kk6-knj-ky1-sumbu-a

‘Macho yanamsumbua.’

(c) *A-me-ruk-w-a* (*na akili*)

kk1-tmlf-ruk-ktndw-kt (na kng10.akili)

- ‘Amerukwa (na akili).’
(d) *A-me-ruk-ik-a* (na akili)*
kk1-tmlf-ruk-ktndk-kt (na kng10.akili)
‘Amerukika (na akili).’
Akili *zi-me-m-ruk-a*
kng9.akili kk10-tmlf-ky1-ruk-kt
‘Akili zimemruka.’

Mfano Na. (10) unaonesha kuwa tungo hizo zimemkweza mmiliki kisha kimilikiwa chake, yaani zimeanza kwa kutaja kitu kizima *yeye* (kiambishi *a-*) kisha kutaja sehemu ya kitu hicho mwishoni mwa tungo *akili* na *macho*. Hii inaashiria kuwa tungo nyingi za aina hii zinahusisha vitenzi vyenye uharibifu katika mwili wa binadamu. Aidha, inaonekana kama vile hakuna kanuni iliyoelezwa kuhusu mhisi kupewa kipaumbele kwa kuwekwa katika nafasi ya juu kabisa katika tungo yaani kiima. Inawezekana ni kwa sababu ya mazoea tu. Hata hivyo, tafiti za uainishaji wa miundo jaribizi, kama zile za Lehmann na wenzake (2004) pia zinathibitisha kuwa kuna mazoea yaliyopitiliza kuhusiana na tabia ya lugha kumfanya mhisi *yeye* (kiambishi *a-*) kama kiima kuliko vipashio vingine. Kwa hiyo, hii ni hali ya kawaida katika Kiswahili hakuna upekee wowote. Hivyo, njia nzuri ya kuaksi kanuni ya ukwezaji wa mmiliki katika tungo zilizo katika mfumo wa aina hiyo ni kutumia tungo za utendwa ambazo zinakubalika zaidi kuliko zile za utendeka katika Kiswahili.

Mbinu ya Kuondoa Utata

Miundo tata ni ya kawaida katika sintaksia. Maarifa ya lugha yanajumuisha kuondoa utata huo katika lugha kwa kutumia mbinu mbalimbali. Kwa mujibu wa SLA, kuna namna mbili katika Kiswahili ambazo zinaweza

kutumika ili kuondoa utata. Namna ya kwanza ni kutumia tungo za utendwa. Namna ya pili ni kwa kutumia urejeshi. Namna zote mbili zinahusisha urejeshaji na mfanano wa virai nomino (Mkude, 2005). Katika Kiswahili, kiashiria cha urejeshi ni kiambishi kinachohusika na kundi la ngeli husika ambacho kinaweza kupachikwa kwa kutumia njia kuu tatu. Kwanza, kinaweza kupachikwa katika kipashio huru kama katika *amba-*, au katika muundo wa kitenzi; mwanzoni au mwishoni mwa muundo wa kitenzi kama inavyoonekana katika Mfano Na. (11).

- (11) (a) *M-toto amba-ye a-na-chek-a ni m-zuri*
kng1-toto amba-krj1 kk1-knj-chek-kt ni kv1-zuri
'Mtoto ambaye anacheka ni mzuri.'
- (b) *M-toto a-na-ye-chek-a ni m-zuri*
kng1-toto kk1-knj-krj1-chek-kt ni kv1-zuri
'Mtoto anayecheka ni mzuri.'
- (c) *M-toto a-chek-a-ye ni m-zuri*
kng1-toto kk1-chek-kt-krj1 ni kv1-zuri
'Mtoto achekaye ni mzuri.'

Mfano Na. (11) unaonesha kuwa miongoni mwa njia hizo tatu, mbinu ya kukiweka kirejeshi katika kipashio *amba-* inakubali kutumika kwa kila tungo bila changamoto yoyote. Hii ni kwa sababu njia hii ina mtawanyiko mkubwa kimatumizi. Njia ya pili nayo ina mtawanyiko mkubwa kidogo kwa sababu kuna hali chache za njeo ambazo hazikubali kufuatiwa na kiambishi rejeshi kabla ya kitenzi. Njia ya tatu ina matumizi finyu kwa sababu haikubali kutokea katika miundo mingi ya vitenzi (Mkude, 2005). Utata ambao ndio kiini cha mjadala wetu hapa unahusiana tu na njia ya pili

ya kukiweka kirejeshi kabla ya mzizi wa kitenzi. Chunguza Mfano Na. (12) kwa ufafanuzi zaidi.

- (12) (a) **Ki-tabu** *ki-me-pote-a*
kng7-tabu kk7-tmlf-pote-kt
'Kitabu kimepotea.'
- (b) *Mw-alimu* *a-li-nunu-a* **ki-tabu**
kng1-alimu kk1-knj-nunu-kt kng7-tabu
'Mwalimu alinunua kitabu.'
- (c) **Ki-tabu** [*mw-alimu a-li-nunu-a* **ki-tabu**] *ki-me-pote-a*
kng7-tabu [kng1-alimu kk1-tmlf-nunu-kt kng7-tabu]
kk7-tmlf-pote-kt
'Kitabu [mwalimu alinunua kitabu] kimepotea'
- (d) **Ki-tabu** *a-li-cho-nunu-a* *mw-alimu* *ki-me-pote-a*
kng7-tabu kk1-knj-krj7-nunua-kt kng1-alimu kk7-tmlf-pote-kt
'Kitabu alichonunua mwalimu kimepotea.'

Kiima cha Mfano Na. (12b) ambayo ni sentesi bebwa 'mwalimu' kimepelekwa mbele ili kuruhusu kiambishi rejeshi *-cho-* ambacho kimepachikwa kabla ya mzizi wa kitenzi *nunua* kuwa karibu na kirejea chake katika Mfano Na. (12d). Endapo hili lisingefanyika, tungo zalishwa isingekubalika kisarufi kama inavyoonekana katika Mfano Na. (13).

- (13) ***Ki-tabu mw-alimu a-li-cho-nunu-a ki-me-pote-a****

kng7-itabu kng1-alimu kk1-knj-krj7-nunu-kt kk7-tmlf-pote-kt

‘Kitabu mwalimu alichonunua kimepotea.’

Mfano Na. (13) unaonesha kuwa kirai nomino ‘*mwalimu*’ kisipopelekwa mbele ili kuruhusu kiambishi rejeshi *-cho-* kupachikwa kabla ya kitenzi *nunua* kuwa karibu na kirejea chake, tungo zalishwa haikubaliki kisarufi kwa sababu inabakia na kiwango fulani cha utata kisemantiki. Kwa upande mwingine, tukitumia mbinu hiyo hiyo ya kukiweka kirejeshi kabla ya mzizi/shina la kitenzi katika tungo itajidhihirisha kama inavyoonekana katika Mfano Na. (14).

- (14) (a) ***Mw-anafunzi a-me-torok-a***

kng1-anafunzi kk1-tmlf-torok-kt

‘Mwanafunzi ametoroka.’

- (b) ***Mw-alimu a-li-m-pig-a mw-anafunzi***

kng1-alimu kk1-knj-ky1-pig-kt kng1-anafunzi

‘Mwalimu alimpiga mwanafunzi.’

- (c) ***Mw-anafunzi [mw-alimu a-li-m-pig-a mw-anafunzi] a-me-torok-a.***

kng1-anafunzi [kng1-alimu kk1-knj-ky1-pig-kt kng1-anafunzi] kk1-tmlf-torok-kt

‘Mwanafunzi[mwalimu alimpiga mwanafunzi] ametoroka.’

- (d) ***Mw-anafunzi a-li-ye-m-pig-a mw-alimu a-me-***

torok-a

kng1-anafunzi kk1-knj-krj1-ky1-pig-kt kng1-alimu
kk1-tmlf-torok-kt

‘Mwanafunzi aliyempiga mwalimu ametoroka.’

Mfano Na. (14) unaonesha kuwa hakuna utata katika tungo zilizotangulia za Na. (13a) & (13b), lakini kuna utata wa wazi katika Mfano Na. (14d) kwa sababu inaweza kumaanisha kuwa *mwalimu alimpiga mwanafunzi* ambayo ndiyo maana tarajiwa katika muktadha huu. Pia inaweza kumaanisha *mwanafunzi alimpiga mwalimu* (ambayo siyo maana iliyotarajiwa lakini kimuundo inawezekana). Kinachosababisha utata katika Mfano Na. (14d) ni ufanano wa kundi la ngeli za nomino zinazohusika: ‘*mwanafunzi*’ na ‘*mwalimu*’ na ukweli kwamba kiambishi rejeshi katika lugha ya Kiswahili hakitofautishi kati ya kiambishi cha kiima na kile cha yambwa kimuundo. Njia pekee ambayo inaweza kuondoa utata katika tungo za namna hii na zingine ni kutumia tungo za utendwa yaani unaigeuza tungo bebwa kuwa katika utendwa kama inavyoonekana katika Mfano Na. (15).

(15) (a) *Mw-anafunzi a-li-ye-pig-w-a (na mw-alimu) a-me-torok-a*

kng1-anafunzi kk1-knj-krj1-pig-ktndw-kt na kng1-alimu
kk1-tmlf-torok-kt

‘Mwanafunzi aliyepigwa (na mwalimu) ametoroka.’

(b) *Mw-anafunzi a-li-ye-pig-ik-a (na mw-alimu) a-me-torok-a**

kng1-anafunzi kk1-knj-krj1-pig-ktndk-kt (na kng1-alimu)
kk1-tmlf-torok-kt

‘Mwanafunzi aliyepigika (na mwalimu) ametoroka.’

Mfano Na. (15a) unaonesha tungo ya utendwa ambayo haina utata ikilinganishwa na ile ya utendeka ya Na. (15b) ambayo ina maana mbili: mwanafunzi ndiye alitoroka na ndiye aliepigwa au mwalimu na mwanafunzi wote wametoroka na wote walipigwa. Halikadhalika, utata mwingine unaonekana katika mfano Na. (16d).

- (16) (a) **Nyumba** *i-me-chaka-a*
kng9.nyumba kk9-tmlf-chaka-kt
‘Nyumba imechakaa.’
- (b) **Kaka** *a-li-m-jeng-e-a* **mama**
nyumba
kng1.kaka kk1-knj-ky1-jeng-ktndea-kt kng1.mama
kng9.nyumba
‘Kaka alimjengea mama nyumba.’
- (c) **Nyumba** [**kaka** *a-li-m-jeng-e-a* **mama nyumba**] *i-me-chaka-a*
kng9.nyumba [kng1.kaka kk1-knj-ky1-jeng-ktndea-kt
kng1.mama kng9.nyumba] kk9-tmlf-chaka-kt
‘Nyumba [kaka alimjengea mama nyumba] imechakaa.’
- (d) **Nyumba** *a-li-yo-m-jeng-e-a* **mama kaka** *i-me-chaka-a*
kng9.nyumba kk1-knj-krj9-ky1-jeng-ktndea-kt
kng1.mama kng1.kaka kk9-tmlf-chaka-kt
‘Nyumba aliyomjengea mama kaka imechakaa’

Data katika Mifano Na. (16a) hadi (16c)) hazina utata isipokuwa katika Mfano Na. (16d), ambapo kuna kufuatana kwa virai nomino viwili ambavyo vinahusu kiumbe hisivu mara tu baada ya kitenzi. Hiki ndicho chanzo cha utata katika tungo hiyo. Hii ni kwa sababu kinadharia, ni vigumu kueleza ni kirai nomino kipi kati ya *mama* na *kaka* kinachorejelea mnufaika, na kipi kinarejelea mtenda. Hata hivyo, tukizingatia kanuni za kisarufi katika lugha ya Kiswahili, virai nomino viwili lazima vitofautishwe kwa kutumia kigezo cha mpangilio na uamilifu wake (Mkude, 2005 na Khamisi, 2008). Kirai nomino kinachotokea mara tu baada ya kitenzi ndicho kinapaswa kurejelea dhima ya mnufaika katika tungo za utenda. Hata hivyo, kigezo cha mpangilio/mfuatano siyo kigezo imara kwa kuwa kuna muktadha ambao mpangilio huo unaweza kubadilika ili kukidhi, kwa mfano, kanuni yenye nguvu/uzito kuliko nyingine (Mkude, 2005 na Philipo, 2017). Ili kuepuka changamoto hiyo, mtumiaji wa lugha, inamlazimu kutumia tungo za utendwa kuliko aina zingine za tungo, ambazo zinaruhusu uhiari wa kupunguza idadi ya vishiriki na kukipa uzito kipashio kinachorejelea mnufaika kama inavyoonekana katika mfano Na. (16e).

(16) (e) *Nyumba a-li-yo-jeng-e-w-a mama (na kaka) i-mechaka-a*

kng9.nyumba kk1-knj-krj9-jeng-ktndea-ktndw-kt

kng1.mama (na kng1.kaka) kk9-tmlf-chaka-kt

‘Nyumba aliyojengewa mama (na kaka) imechakaa.’

Data Na. (16e) inaonesha kuwa aina hii ya utata hutokea mara nyingi katika vitenzi vyote vielekezi vyenye miundo ya vishiriki vitatu ambapo yambwa

inafanywa kisabiki cha kishazi rejeshi. Tungo za utendwa kwa hiyo ndiyo njia pekee na nzuri ya kuondoa utata katika mazingira hayo ya utokeaji wa tungo hizo kimawasiliano kuliko zile za utendeka. Ni muhimu kusisitiza hapa kwamba changamoto zilizojitokeza katika tungo hizo zisingetokea kama njia ya kuunda urejeshi kwa kutumia kipashio *amba-* ingetumika. Aidha, badala ya kutumia utendwa, inawezekana pia kutumia njia ya kukipachika kirejeshi katika kipashio *amba-*.

Ufokalishaji wa Mtenda

Ufokalishaji wa mtenda ni mchakato wa kisintaksia, ambapo mtenda katika tungo anawasilishwa kama taarifa mpya isiyojulikana na ambayo huwasilishwa na kusisitizwa kwa mpokeaji kwa mujibu wa SLA, hususani muundo wa taarifa. Kimawasiliano, lengo la ufokalishaji huo ni kuweka wazi taarifa inayomhusu mtendaji wa tendo kama taarifa mpya katika tungo. Taarifa ya aina hii, awali, haijulikani kwa mpokeaji bali inajulikana kwa mtoaji wa taarifa tu. Uchunguzi umebaini kwamba, tungo za utendwa zina lengo la kumfanya mtendaji wa tendo katika tungo kuwa taarifa mpya ambayo inawasilishwa na kusisitizwa katika tungo. Hivyo, mtumiaji wa lugha ikiwa atahitaji kuwasilisha taarifa ambayo inamhusisha mtendaji wa tendo katika tungo kama fokasi kimawasiliano, itamlazimu kutumia tungo za utendwa ambazo muundo wake unaruhusu kurejeshwa kwa mtenda huyo katika tungo kama chagizo. Hili linafanyika ili kukidhi haja ya mawasiliano yanayofanyika.

Uelewa wa jumla ni kwamba tungo za utendeka na utendwa zinaondoa kishiriki ambacho kina dhima ya mtenda katika MVSH vya kitenzi (Rugemalira, 1993 na Kaoneka, 2009). Upekee wa sintaksia ya kila lugha

unapaswa kupewa kipaumbele, kuzingatiwa na kutambuliwa. Hii ni kwa sababu utendwa katika Kiswahili unadhibiti idadi ya vishiriki au kupunguza kutegemeana na muktadha wa mawasiliano. Katika lugha ambazo ufokalishaji unaweza kufanyika kwa kuhamisha vipashio kwa kuvipeleka mwanzoni au mwishoni mwa tungo, mara nyingi, huchukuliwa kwamba kumtaja mtendaji wa tendo katika tungo ni suala la ufokalishaji kama inavyoonekana katika Mfano Na. (17).

- (17) (a) ***M-toto*** *a-me-vunj-a* *ki-ti*
Kng1-toto kk1-tmlf-vunj-kt kng7-ti
'Mtoto amevunja kiti.'
- (b) *Ki-ti* *ki-me-vunj-w-a* (***na m-toto***)
kng7-ti kk7-tmlf-vunj-ktndw-kt (na kng1-toto)
'Kiti kimevunjwa (na mtoto).'
- (c) *Ki-ti* *ki-me-vunj-ik-a* (***na m-toto***)*
kng7-ti kk7-tmlf-vunj-ktndk-kt na kng1-toto
'Kiti kimevunjika (na mtoto).'

Mfano Na. (17a) unaonesha tungo ya utendwa yenye kiambajengo kinachorejelea mtendaji wa tendo *mtoto* katika tungo kama mada na kiti ni *fokasi*. Aidha, Mfano Na. (17b) unaonesha tungo ya utendwa. Katika tungo hii, mada ni kiathirika *kiti* na fokasi ni mtenda *mtoto*. Tungo hii inajitokeza iwapo mtendaji wa tendo *mtoto* ni taarifa mpya inayosisitizwa katika tungo. Katika utafiti tulioufanya, imebainika kwamba, mtendaji wa tendo anadokeza taarifa mpya kama anahusishwa na taarifa inayoulizwa katika tungo. Kama mtendaji wa tendo ndiye anayehusishwa na taarifa inayoulizwa, atajitokeza baada ya kitenzi katika tungo. Aidha, tungo ya utendeka katika Mfano Na. (17b) haikubali kuambatana na dhima hiyo

kama fokasi katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kutokana na muundo wake wa vishiriki ambao hauruhusu kutokea pamoja na mtenda huyo.

Katika Kiswahili na katika lugha zingine za Kibantu, swali linalohusu kiambajengo kinachorejelea kiima (mtenda) katika tungo linajitokeza na kuulizwa wakati wote, na mara nyingi linafanyika kwa kutumia uhamishaji wa vipashio kutoka mwishoni kwenda mwanzoni mwa tungo. Ni jambo la kawaida na rahisi katika hali kama hiyo kujibu swali hilo kwa kutumia tungo za utendwa na kukitaja kiambajengo kinachoulizwa katika muundo wa tungo kama ilivyooneshwa katika Mfano Na. (18).

- (18) (a) *A-li-ye-ku-fundish-a* *w-imbo huo (ni) nani?*
kk1-knj-krj1-ky1-fundish-kt kng9-imbo huo (ni)
nani?
'Aliyekufundisha wimbo huo ni nani?
Ni-li-fundish-w-a (*na bibi*)
'kk1-knj-fundish-ktndw-kt (na kng1.bibi).'
'Nilifundishwa (na bibi).'
- (b) *A-li-ye-ku-elekez-a* *nyumba-ni kw-angu ni nani?*
kk1-knj-krj1-ky1-elekez-kt kng9.nyumba-ktm kv-
17-angu ni nani?
'Aliyekuelekeza nyumbani kwangu ni nani?'
Ni-li-elekez-w-a (*na dada*)
kk1-knj-elekez-ktndw-kt (na kng1.dada)
'Niliekezwa (na dada).'

Ni wazi kwamba katika Kiswahili siyo jambo la kawaida ama kwa swali lenyewe kuwa katika muundo wa utendwa kama inavyoonekana katika Mfano Na. (19).

- (19) (a) *Habari hi-yo u-me-ambi-w-a na nani?*
kng9.habari kv9-hiyo kk1-tmlf-ambi-ktndw-kt na
nani?
'Habari hiyo umeambiwa na nani?'
- (b) *Ni-me-ambi-w-a (na ma-jirani)*
kk1-tmlf-ambi-ktndw-kt na kng2-jirani
'Nimeambiwa na majirani.'
- (c) *U-na-it-w-a!*
kk1-knj-it-ktndw-kt!
'Unaitwa!'
- (d) *Ni-na-it-w-a na nani?*
kk1-knj-it-ktndw-kt na nani?
'Ninaitwa na nani?'
- (e) *U-na-it-w-a (na mw-alimu)*
kk1-knj-it-ktndw-kt (na kng1-alimu)
'Unaitwa (na mwalimu)'

Tungo zilizomo katika Data Na. (19) zinadhihirisha kuwa tungo za utendwa zinatumiwa kwa lengo la ufokalishaji wa mtenda ambaye anapelekwa mwishoni mwa tungo baada ya kitenzi kiundacho tungo husika. Kimawasiliano, ufokalishaji wa mtenda unabainisha kuwa taarifa mpya ambayo haijulikani kwa mpokeaji katika tungo inahusu mtendaji wa tendo. Sababu ya ufokalishaji huo ni kuwezesha mawasiliano baina ya mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Aidha, ikumbukwe kwamba ufokalishaji ni dhana pana

kuliko utendwa. Utendwa ni sehemu moja tu ya ufokalishaji. Inawezekana kufokalisha kirai nomino chochote bila kuhusisha utendwa. Mathalani, ufokalishaji unaweza kufanyika pia kwa kutumia mchakato wa upinduzi wa kimahali au ukwezaji wa mmiliki kutegemea muktadha wa kisarufi na kimawasiliano ambamo tungo husika inajitokeza (Mkude, 2005 na Hassan, 2019). Hivyo, uchunguzi umebaini kwamba, tungo za utendwa zina lengo la kumfanya mtendaji wa tendo katika tungo kuwa taarifa mpya ambayo inasisitizwa katika tungo.

Umadaishaji wa Kiathirika/Kithimu

Umadaishaji wa kiathirika au kithimu ni mchakato wa kisintaksia unaokikweza kiumbe ambacho ni kiathirika au kithimu na kukihamishia katika nafasi ya kiima katika tungo, na kuwasilishwa kama taarifa ya zamani inayofahamika kwa mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Kimawasiliano, umadaishaji wa kiathirika au kithimu unasaidia kuweka wazi taarifa inayofahamika kwa mtoaji na mpokeaji wa ujumbe kwamba ni kuhusu kiathirika au kithimu. Lengo la umadaishaji huo ni kufanikisha mawasiliano baina ya mtoaji na mpokeaji wa taarifa katika muktadha husika wa mawasiliano kwa mujibu wa SLA, hasa muundo wa taarifa.

Kwa kawaida, kiima katika tungo ndicho kinadokeza taarifa ambayo ni mada katika lugha za Kibantu. Ikiwa tungo inahusisha viambajengo zaidi ya kimoja, uchaguzi wa kishiriki kipi kiwe kiima lazima ufanyike. Uchaguzi huo uzingatie hadhi na nafasi ya dhima ya kisemantiki ya kishiriki hicho katika msonge wa dhima za kisemantiki na muktadha wa mawasiliano. Kinadharia, kishiriki kinachorejelea dhima ya kisemantiki ilyopo katika nafasi ya juu kuliko kishiriki kingine lilichoko katika nafasi ya chini katika msonge wa dhima za kisemantiki, ndicho kinapaswa kuwa kiima. Kwa

mfano, mtendaji wa tendo anapokuwa ndiye amepewa umuhimu wa juu katika tungo na vishiriki vingine vinafuata baada ya mtenda, hivyo, mtenda ndiye atapewa hadhi ya kuwa kiima katika tungo husika. Aidha, mchakato wa tungo za utendwa hutumika kushusha hadhi kiambajengo chenye dhima ya juu katika msonge na kukihamishia katika nafasi ya chini kimuundo katika tungo, yaani kishiriki ambacho siyo mtendaji wa tendo katika tungo ndicho kinapewa umuhimu wa juu kuliko vishiriki vingine. Hata hivyo, dhana ya umuhimu wa juu inamaanisha nini? Aissen (1999) anaeleza kuwa zipo sababu kuu mbili zinazokifanya kishiriki kuwa na umuhimu mkubwa kuliko vingine katika tungo:

Kwanza, ni umadaishaji, ambapo kishiriki kiini (msingi) katika mawasiliano ndicho hupewa umuhimu mkubwa kuliko vishiriki vingine. Pili, ni kishiriki ambacho kimeshatajwa katika tungo zilizotangulia katika mawasiliano. Kishiriki hicho, kwa kawaida, hupewa umuhimu zaidi kuliko vishiriki vingine ambavyo havijatajwa katika matini zilizotangulia kulingana na muktadha wa mawasiliano. Hii ni kwa sababu, kinawasilisha taarifa ya zamani inayofahamika kwa mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Hoja ya msingi hapa ni kwamba, uchaguzi wa yambwa kuwa kiima utategemea kiini cha mawasiliano ni nini kutegemea muktadha wa mawasiliano. Kama kiini cha mawasiliano ni yambwa, basi, yambwa ndiyo itakuwa kiima.

Hivyo, kisintaksia, kishiriki kinachokuwa kiima katika tungo ndicho hupewa hadhi na umuhimu wa juu kuliko vishiriki vingine. Aidha, mpangilio wa viambajengo katika tungo siyo wa asili kama ambavyo inadhaniwa kinadharia, bali ni wa kimuktadha. Katika Kiswahili, kwa mfano, kitenzi chenye muundo wa vishiriki viwili, mtenda na kiathirika, yambwa ndiyo huwa kiima cha tungo za utendwa. Katika tungo zenye

vitenzi vyenye muundo wa vishiriki vitatu, yambiwa ndiyo huwa kiima cha tungo za utendwa. Aidha, umadaishaji ni dhana pana kuliko utendwa. Utendwa ni sehemu moja tu ya umadaishaji. Upo uwezekano wa kumadaisha kishiriki bila kuhusisha utendwa. Ingawa yambwa katika vitenzi vyenye vishiriki vitatu haiwezi kuwa kiima cha tungo tendeka wala tendwa. Hata hivyo, bado upo uwezekano wa kumadaishwa kwa kutumia ama mchakato wa upinduzi wa kimahali au ukwezaji wa mmiliki.

Kwa mujibu wa data zilizotumika katika makala hii, imebainika kwamba tungo za utendeka na zile za utendwa matumizi yake yanaukiliwa na umadaishaji wa kiathirika au kithimu. Sababu ya umadaishaji huo ni kuweka wazi taarifa inayohusu kiathirika au kithimu ambayo mtoaji wa taarifa anadhani kwamba mpokeaji naye anaifahamu kwa lengo la kuwezesha ujumbe uliokusudiwa na mtoaji kumfikia mpokeaji kikamilifu. Mchakato huu unatokea ikiwa kiathirika au kithimu kinadokeza taarifa ya zamani ambayo ama imetajwa hapo awali katika tungo au inafahamika kwa wote yaani mtoaji na mpokeaji wa taarifa kutokana na muktadha wa mawasiliano. Hivyo, katika muktadha kama huo, tungo za utendwa ndizo hutumika zaidi kutokana na muundo wake wa vishiriki kuwa na vishiriki zaidi ya kimoja yaani kiathirika au kithimu na mtenda ikilinganishwa na tungo za utendeka ambazo huwa na kiathirika au kithimu tu. Hapa tungo za utendwa hutumika ambapo kishiriki kinachorejelea kiathirika au kithimu kinatokea katika nafasi ya kiima kabla ya kitenzi katika tungo (Rugemalira, 1993; Seidl na Dimitriads, 2003; na Mkude, 2005). Hali kadhalika, kiathirika au kithimu hicho hudokeza taarifa ambayo ni mada katika tungo na mtenda hufanywa chagizo kama inavyoonekana katika Mfano Na. (20).

(20) (a) *Baba a-me-jeng-a nyumba*

Kng1.baba kk1-tmlf-jeng-kt kng9.nyumba

‘Baba amejenga nyumba.’

(b) *Nyumba* *i-me-jengek-a (na baba)**

Kng9.nyumba kk9-tmlf-jeng-ktndk-kt na

kng1.baba

‘Nyumba imejengeka (na baba).’

(c) *Nyumba* *i-me-jeng-w-a (na baba)*

kng9.nyumba kk9-tmlf-jeng-ktndw-kt (na

kng1.baba)

‘Nyumba imejengwa (na baba).’

Mfano Na. (20a) unaonesha tungo ya utenda ambayo mada ni *baba* na fokasi ni *nyumba*. Mfano Na. (20b) unaonesha tungo ya utendeka ambayo haikubaliki. Mfano Na. (20c) unaonesha tungo ya utendwa. Katika tungo hiyo, mada ni kiathirika au kithimu *nyumba* na siyo mtenda *baba*. Tungo hizo hutokea iwapo kiathirika au kithimu *nyumba* ni taarifa inayofahamika kwa mtoaji na mpokeaji wa taarifa katika muktadha wa mawasiliano. Aidha, kiathirika au kithimu kinaweza kudokeza taarifa inayofahamika kwa sababu kimetajwa na kutokea katika sentensi zilizotangulia katika matini.

Kwa hiyo, tungo za utendwa zina matumizi mapana kimawasiliano ikilinganishwa na zile za utendeka. Hii ni kutokana na MVSH wa tungo hizo katika lugha ambao unahusisha dhima ya mtenda kama chagizo. Ni muhimu kutambua kuwa, utendwa ni mojawapo tu ya miundo kadhaa ya tungo ambazo kishiriki chenye hadhi ya juu katika msonge wa dhima za kisemantiki kinashushwa hadhi ili kuruhusu vishiriki vingine vilivyoko katika nafasi ya chini katika msonge wa dhima za kisemantiki kuchukua

nafasi ya juu na kuwa kiima katika tungo (Rugemalira, 2005; Mkude, 2005; na Lusekelo, 2012). Aidha, tungo mbalimbali za upinduzi wa kimahali pamoja na zile za ukwezaji wa mmiliki zinashiriki baadhi ya sifa za tungo za utendwa katika lugha. Tungo hizo pamoja na tungo za utendwa zinawezesha lugha kuwa na uwezo wa kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati au maendeleo ya sayansi na teknolojia ili kuendana na changamoto za mawasiliano yasiyokuwa rasmi (mazungumzo) katika jamii ya sasa. (Mkude, 2005).

Hitimisho

Katika makala hii tumebainisha na kufafanua sababu zinazoukilia matumizi ya tungo za utendeka na utendwa. Kwa kutumika mkabala wa SLA tumeweza kubainisha na kufafanua sababu mbalimbali zinazoukilia utumikaji wake katika muundo wa lugha. Ufafanuzi huu umebainisha kuwa tungo za utendeka na utendwa hazitumiki kiholela. Halikadhalika, zina miundo mbalimbali inayotoa taarifa tofauti kwa kadri ya miundo ya tungo hizo. Imedhihirika pia kwamba, kadri miundo ya tungo hizo inavyobadilika ndivyo na uamilifu wake pia kimawasiliano unavyobadilika. Mabadiliko ya miundo mbalimbali ya tungo yanakidhi haja ya ufafanuzi wa Nadharia ya SLA inayosisitiza kuwa tungo ina miundo ambajengo na miundo amilifu. Kutokana na matokeo hayo, inapendekezwa kwamba, utafiti zaidi kama huu ufanyike katika lugha zingine za Kibantu ambazo hazijafanyiwa utafiti ili kulinganisha na kutofautisha sababu za utumikaji wake katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.

Marejeleo

- Aissen, J. (1999). “Markedness and Subject Choice in Optimality Theory”. *Natural language and Linguistic Theory*, 17 (4), 673 - 711.
- Bresnan, J. na Kaplan, R.M. (1982). Lexical-Functional Grammar: A Formal System for Grammatical Representation. Katika J. Bresnan (Mh.), *The Mental Representation of Grammatical Relations* (uk. 173 -281).Cambridge: The MIT Press.
- Bresnan, J. na Kanerva, J.M. (1989). Locative Inversion in Chichewa: A Case Study of Factorization in Grammar. *Linguistic Inquiry*, 20, 1 - 50.
- Chafe, W.L. (1976). Givenness, Contrastiveness, Definiteness, Subject, Topic, and Point of View. Katika C. Li (Ed.), *Subject and Topic* (uk. 25 - 55). New York: Academic Press.
- Givon, T. (2001). *Syntax: An Introduction*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.
- Hassan, F. (2019). *Uchanganuzi wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kaoneka, S. (2009). *Verb Extension in Shambala: Their Occurrence and Co-occurrence Constraints* (Unpublished Master’s Dissertation). University of Dar es Salaam.
- Keenan, E. L. (1976). Towards a Universal Definition of Subject. Katika C. N. Li, (Ed.), *Subject and Topic* (30 - 333). New York: Academic Press.
- Khamisi, M.A. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. University Press.
- Lambrecht, K. (1994). *Information Structure and Sentence Form: Topic, Focus and Mental Representation of Discourse Referents*. Cambridge University Press.

- Lehmann, C. na Wenzake. (2004). *Person Prominence and Relation Prominence: On Typology of Syntactic Relations with Particular Reference to Yucatec Maya*. Universitat Erfurt, Faculty of Philosophy. No. 12.
- Mkude, D.J. (2005). *The Passive Constructions in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).
- Reinhart, T. (1981). Pragmatics and Linguistics: An Analysis of Sentence Topics. *Philosophica*, 27, 53 - 94.
- Rugemalira, J. (1993). *Runyambo Verb Extension and Constraints on Predicate Structure* (Unpublished PhD Thesis). University of California in Barkley, California.
- Scotton, C.M.M. (1967). Semantic and Syntactic Subcategorization in Swahili Verb Shapes. *Journal of African Linguistics* 12.172 - 182.
- Seidl, A. na Dimitriads, A. (2003). *Statives and Reciprocal Morphology in Swahili*. Katika Patric Sauzet and Anne Zribi-Hertz (Ed) *Typologie des Langues d: Afrique et Universax* University Paris.